



## **MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

### **TAARIFA KWA UMMA UFAFANUZI KUHUSU WAAJIRIWA KUWA NA NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN)**

***Dar es Salaam, 18 Agosti, 2020:***

Mamlaka ya Mapato Tanzania ("TRA" au "Mamlaka") inapenda kutoa ufanuzi kuhusu waajiriwa kuwa na Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) kama ifuatavyo:-

Kwamba mnamo tarehe **6 Agosti 2020**, Mamlaka ilizindua mfumo wa uwasilishaji ritani za kodi kwa njia ya mtandao (**e-Filing**) ambapo, pamoja na ritani zingine, mfumo huu unajumuisha ritani ya zio katika mapato ya waajiriwa, yaani, Pay As You Earn (PAYE).

Kutokana na mabadiliko hayo kuanzia sasa kila mwajiri atalazimika kuwasilisha ritani ya zio katika mapato ya waajiriwa (PAYE) ikioneshwa namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN) ya kila mwajiriwa na kodi husika iliyokatwa.

Kwa waajiriwa ambao TIN tayari wanazo, mwajiri ataziingiza katika ritani zake kuonesha kiasi cha kodi kilichokatwa kwa mwajiriwa husika na kuwasilishwa TRA.

Aidha, kwa waajiriwa ambao kwa sasa hawana TIN, na kwamba ama wana Kitambulisho cha Taifa kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) au Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIN), wanaelekezwa kuomba TIN hizo kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa **Online TIN Registration** unaopatikana kwenye tovuti ya TRA (ambao ni [www.tra.go.tz](http://www.tra.go.tz)). Kwa waajiriwa wasio na Kitambulisho cha Taifa watalazimika kutembelea Ofisi za TRA kupigwa picha na kuchukuliwa alama za vidole.

Hata hivyo, waajiri wanaelekezwa kuwa kwa waajiriwa ambao kwa sasa hawana TIN, waajiri wataingiza namba ya TIN ya mfano ambayo ni **999 999 999** wakati wa kuwasilisha ritani za kodi ya ajira kwa ajili ya kuwezesha kushughulikia mishahara yao.

## **Uk. 2**

Vile vile, tunapenda kufafanua kwamba ukomo wa utaratibu huu kwa wasio na TIN ni hadi mnamo tarehe **31 Desemba 2020**. Baada ya hapo hakutokuwa na muda wa nyongeza. Hivyo, tunawaomba na kuwasih i waajiri na waajiriwa wote wajitahidi kutekeleza wajibu wao katika muda uliowekwa hasa ikizingatiwa kuwa mlipakodi anapaswa kuwa na TIN ikiwa ni matakwa ya **Kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 R.E 2019**.

Kwa maelezo zaidi; unaweza kutembelea Ofisi ya Mamlaka iliyo karibu nawe. Pia, unaweza kutembelea tovuti ya TRA ([www.tra.go.tz](http://www.tra.go.tz)) au kupiga simu bure kuitia **0800 750 075** au **0800 780 078**, na kutuma ujumbe wa WhatsApp (**0744 23 33 33**) au kutuandikia barua pepe kwa anwani pepe [huduma@tra.go.tz](mailto:huduma@tra.go.tz) au [services@tra.go.tz](mailto:services@tra.go.tz).

***“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”***

Imetolewa na;

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI  
TRA MAKAO MAKUU**